



IFAHAMU SUMU KUVU



SUMUKUVU ni sumu/kemikali zinazozalishwa na aina za fangasi /ukungu/kuvu wanaoota kwenye punje za nafaka, mbegu za mafuta, mikunde na mazao ya mizizi kama vile karanga wakati yakiwa shambani au katika sehemu ya kutunzia (ghala).

Ingawa aina nyingi za kuvu zinaweza kuota na kukua katika vyakula, ni aina chache tu za kuvu (**fangasi**) amabao hutoa sumu kuvu. Endapo vayakula anavyokula binadamu au mnyama vina sumu kuvu nyingi afya zao hudhurika kwa kiwango cha juu. Sumu kuvu **haionekani kwa macho, haina harufu, haina kionjo, wala rangi**, lakini kuvu anayetoa sumu hizo anaweza kuwa na rangi ya **kijani, chungwa**, kijivu au njano chafu na anaweza kutoa harufu ya uvundo. **SUMUKUVU** pia hupatikana katika bidhaa za mifugo kama vile mayai, nyama na maziwa iwapo watakula chakula kilichochofuliwa na sumu. Pia hupatikana katika maziwa ya mama anayenyonyesha iwapo atakula chakula chenye sumu kuvu

Dalili za Sumukuvu kwa binadamu

Binadamu aliyekula chakula chenye sumukuvu huonyesha dalili kama maumivu ya tumbo, kutapika, kuvimba tumbo, homa, kuharisha, kuwa wa njano sehemu mbalimbali za mwili (nyayo, viganya vya 2 mikono na miguu), kujaa maji kwenye mapafu na degedege. Uonapo dalili hizo ni vema kuwahi katika kituo cha kutolea huduma za afya.

Madhara yatokanayo na sumu kuvu

Madhara yatokanayo na sumukuvu yako ya aina mbili. Kuna madhara yanayojitokeza baada ya muda mfupi na madhara yanayojitokeza baada ya muda mrefu. Madhara ya muda mfupi au mrefu hutegemea kiasi cha sumu kuvu kwenye chakula kilicholiwa, muda ambao chakula kilichochofuliwa kimekuwa kikitumika, umri wa mlaji na hali ya kiafya kwa ujumla. Ikumbukwe kwamba watoto wadogo, watu wenye kinga mwili duni na hali ya lishe duni huathirika zaidi.

Kama chakula au kinywaji chenye sumu kuvu kitatumiwa na binadamu au mnyama ataugua kwa kutegemea na kiasi cha sumu kuvu kilichomo. Vyakula ambavyo vinaweza kuambukizwa sumu kuvu ni kama vile mahindi na unga wake, karanga na mazao yanayotokana na karanga, muhogo, nyama, mayai na maziwa (vitokanavyo na mnyama au ndege aliyeambukizwa pamoja na mazao yao) na vyakula vya mifugo (vyenye mbegu zilizoambukizwa au nyasi au vyaluka vya mifugo vya kutengenezwa). Saratani, hasa ya ini, kushusha kinga ya mwili, kudumaa hasa kwa watoto, sumu kwenye figo na vifo kwa binadamu na wanyama ikiwa viwango vya sumu kuvu ni vikubwa. Baadhi ya sumu kuvu hutoka kwa mama kwenda kwa mtoto akiwa bado tumboni. Kutokana na madhara ya afya yanayosababishwa na sumu kuvu kwa binadamu na wanyama sumu kuvu haziruhusiwi kuwepo katika mazao yaliyokusudiwa kwa biashara na kama zikigunduliwa katika mazao ya kilimo hayatauzika na badala yake yatateketzwa. Kwa kiwango kikubwa sumu kuvu huathiri biashara, faida na afya za wazalishaji.

Njia za kudhibiti maambukizi ya sumu kuvu

- Lima aina za mazao zenye ukinzani dhidi ya kuvu wanaotoa sumu kuvu (kama aina hizo zinapatikana)
- Vuna mazao yakiwa yamekauka vizuri kama inavyoshauriwa na bwana/bibi shamba na epuka kutia majeraha kwenye mazao yako
- Usianike mazao yako kwenye udongo mtupu. Anika sehemu iliyoinuka kama meza na utumie turubai au aina nyingine ya kifaa cha kuanikia
- Wakati na baada ya kuvuna tupa mbegu au mazao yaliyooza
- Hifadhi mazao mahali pakavu na pasipo na joto. Hakikisha mazao yaliyohifadhiwa hayalowi
- Ghala liruhusu mzunguko wa hewa, zuia wadudu waharibifu na kuvu kwa kunyunyiza madawa yaliyokubalika na kushauriwa
- Kama yanapatikana, tumia madawa ya kibayologia kama vile AflaSafe™ (aina ya kuvu ambaye hukinzana na yule atoaye sumu kuvu)
- Tumia madawa yanayodhibiti na kuondoa sumu kuvu wakati wa usindikaji wa vyakula vya binadamu na vile vya wanyama



IMEANDALIWA NA **BENJAMIN K MWENDA** KUTOKA **TANGANYIKA FARMERS ASSOCIATION (TFA)**, ARUSHA- TANZANIA- www.tfa.co.tz

TFA Head Office: Arusha Shule Plot, TFA -Plot 76 Block E School Road Arusha

P.O. Box 3010 ARUSHA-Tanzania | Web: www.tfa.co.tz